

**MAAZIMIO YA KIKAO KAZI CHA TATU (3) CHA MAMLAKA YA SERIKALI
MTANDAO KILICHOFANYIKA TAREHE 08 – 10 FEBRUARI, 2023**

Yafuatayo yalikuwa maazimio kumi na mawili (12) ya kikao kazi cha tatu (3) cha Serkali Mtandao cha mwaka 2023:

1. Taasisi za Umma ziwajibike kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utoaji wa huduma kwa wananchi kwa njia ya kidijitali ili kuboresha utendaji kazi wa Taasisi za Umma.
2. Taasisi za Umma zihakikishe zinaendesha shughuli za kawaida za taasisi kama vile uendeshaji wa vikao vya menejimenti, vikao vya bodi, vikao vya halmashauri na vikao vya mabaraza ya madiwani kidijitali ili kupunguza matumizi ya karatasi.
3. Kila Taasisi ya Umma ihakikishe tovuti ya taasisi inakuwa na taarifa zilizohuishwa na zinazoendana na wakati muda wote. Pia Tovuti hizo ziboreshwe ili kuendana na teknolojia za kisasa.
4. Taasisi za umma zitoe kipaumbele katika masuala ya utafiti na ubunifu kwenye eneo la TEHAMA ili kuibua mifumo ya TEHAMA itakayowezesha taifa kuendana na kasi ya maendeleo ya viwanda (4th Industrial Revolution), ikiwemo kutenga rasilimali fedha kwa ajili ya ubunifu.
5. Mamlaka ya Serkali Mtandao (e-GA) kwa kushirikiana na Taasisi za Umma iendelee kujenga Mifumo shirikishi na mifumo ya kisekta katika jitihada za kupunguza urudufu wa Mifumo ya TEHAMA katika utumishi wa umma.
6. Wakuu wa Taasisi za Umma wanalazimika kujiunga kwenye Mfumo Mkuu wa Serikali wa kubadilishana taarifa (Government Enterprise Service Bus - GovESB) ili kuwezesha mifumo kubadilishana taarifa.
7. Taasisi za Umma zinalazimika kuhifadhi Mifumo yao kwenye vituo vya kuhifadhi data vya Serikali vilivyoidhinishwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ili kupunguza gharama na kuongeza usalama. Aidha, Usalama wa mifumo iliyokwishajengwa uendelee kuimarishwa ikiwa ni pamoja na kuwa na Vituo vya Kujikinga na Majanga (*redundancy*)
8. Wakuu wa taasisi za Umma wasimamie kikamilifu Utekelezaji wa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019 na Kanuni zake za Mwaka 2020 hasa uanzishwaji wa Kamati ya Uongozi wa TEHAMA (Institutional ICT Steering Committee) na kusimamia utendaji kazi wa kamati hizo.

9. Serikali ianzishe utaratibu wa kuwafanyia upekuzi pamoja na matamko ya kiapo kwa watumishi wa TEHAMA kwa kuwa wanasimamia mifumo na data nyeti za Serikali.
10. Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi iweke mkakati wa kuwaandaa wanafunzi wa Vyuvo vya elimu ya juu katika kufanya ubunifu katika masuala ya Serikali Mtandao na TEHAMA kwa ujumla.
11. Serikali iwekeze katika kuanza kutengeneza vifaa vya TEHAMA hapa nchini.
12. Mifumo ya TEHAMA ya Serikali inayojengwa iwe endelevu (sustainable) ili kuepuka kubadilisha mifumo mara kwa mara kwa kuwa hadi mfumo kuanza kutumika kunakuwa na uwekezaji mkubwa, ikiwemo mafunzo kwa watumiaji.